

## **LBE 2009 – Migration**

### **Episode 8**

#### **Going Home: Ghana - Somalia**

**Author:** Bettina Rühl

**Editor:** Thomas Mösch

**Translator:** Anne Thomas

#### **Characters:**

##### **Scene 1:**

**Narrator** (female)

**Edmund Mbroso** (male, in his early 30s, English)

---

##### **Scene 2:**

**Narrator** (female)

**Guled Abdisalam** (male, 32, English)

---

#### **Intro:**

Hujambo na karibu tena kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu Uhamiaji kati ya Afrika Na Ulaya. Leo kwa mara nyingine tena tunaangazia juu ya Waafrika waliorudi nyumbani baada ya kuishi Ulaya kwa muda. Karibu tuandamane pamoja hadi Ghana na Somalia.

---

## **Scene 1:**

### **1. SFX The depot of a meat importing company in Tema, Ghana**

#### **2. Narrator:**

Tupo katika kampuni ya kusafirisha nyama kwenye eneo la viwanda la Tema. Tema ni bandari muhimu nchini Ghana, huko Afrika Magharibi. Kuna alama ya maandishi ukutani yaliyoandikwa: "Adom Mbroso Import-Export". Wanawake wanapakia maboksi kwenye masanduku. Maboksi hayo yanaangukiana kwa kishindo – bidhaa hizo zimeganda ndio maana ni ngumu kama jiwe.

### **3. SFX: in the offices of the meat importing company, Tema, Ghana**

#### **4. Narrator:**

Mkurugenzi mkuu wa kampuni amekaa mezani kwake. Inashangaza kwani ni kijana mno. Anajitambulisha kuwa anaitwa Edmund na anasema anaendesha kampuni hiyo ya Adom Mbroso kampuni ya kusafirisha na kuingiza bidhaa.

### **5. SFX: at the cold-storage depot**

#### **6. Narrator:**

Kampuni hiyo inashughulikia bidhaa zilizogandishwa kwenye barafu – hususan nyama na samaki. Nyama ya nguruwe kutoka Uholanzi na Ujerumani, kuku kutoka Brazil, samaki kutoka Mauritania, kimsingi nyama na samaki wa kila aina kutoka kila pembe duniani. Kampuni hiyo ina tawi lake huko Kumasi, sehemu ya ndani ya nchi. Edmund anaeleza kwamba kampuni yake imewaajiri takriban wafanyakazi 100 wa kudumu huko Tema peke yake na pia ina vibarua karibu 250. Kwa hivyo kampuni

hiyo si ndogo. Bila shaka mkurugenzi huyo mkuu mwenye umri wa miaka 30 ana majukumu makubwa. Hasa wakati huu ambapo uchumi wa dunia unayumba.

### **7. O-Ton Edmund Mbroso**

Kwa hakika, viwango vya uuzaji vimeanguka sana. Zamani tulikuwa tunauza, tuseme kontena tano za nyama ya kuku katika mwezi mmoja, hivi sasa ni bahati pia tukiuzua kontena moja, ambayo ina tani 20. Kwa hivyo kutoka kwenye tani zaidi ya 120 hadi tani 28 – mauzo yetu yameanguka sana na kila mahala hali ni kama hiyo! Kila unayezungumza naye unakuta na yeye amekumbwa na hali kama hiyo!

### **8. Narrator:**

Hata ingawa Edmund anazungumza kwa utulivu, hali halisi haitoi ishara nzuri. Kwa hakika, hali ni mbaya. Alipoulizwa iwapo ana wasiwasi na hali ya baadaye, anajibu kwa dhati:

### **9. O-Ton Edmund Mbroso**

Kusema kweli, hakuna matarajio! Kila mara kuna hili au lile – kama si mgogoro wa uchumi basi itakuwa mgogoro wa mafuta, gharama ya kufanya biashara nchini Ghana ni ya juu mno. Na ninavyoona mimi ni kwamba sera za serikali hazisaidii kitu.

### **10. Narrator:**

Hali kama hii inawalazimisha maelfu ya waafrika kujaribu bahati zao hapa Ulaya kila mwaka. Lakini sio Edmund. Ndio kwanza amerudi:

### **11. O-Ton Edmund Mbroso**

Niliishi London kama miaka 10 hivi. Nimepata elimu yangu ya juu huko huko London, nimesomea chuo kikuu na kila kitu, nimepata shahada yangu ya uzamili, na nilikuwa napata fedha nzuri tu, lakini nimerudi nyumbani ili kusaidia. Hiki ni kitu changu binafsi. Kule London, nilikuwa nimeajiriwa serikalini, kwa hivyo siwezi kusema ilikuwa vizuri kuliko hapa, nina maana nikifanya kazi kwa bidii na hii biashara ikinawiri vizuri nitakuwa nimefanya kitu changu binafsi sio cha serikali. Huko London, nilifanya kazi kwa bidii sana lakini serikali ilinilipa mshara mwisho wa mwezi tu, na ndio maana nikaamua kurudi nyumbani.

## **12. Narrator:**

Kusema kweli, hali ya Edmund inaonyesha kuwa nzuri kuliko hali ya Waghana wengi. Wazazi wake walianzisha kampuni hiyo ya kusafirisha na kuingiza mizigo ambayo yeye sasa anaiendesha. Wazazi wake ni wazee na hawana tena nguvu za kusimamia kampuni peke yao – hasa katika nyakati hizi ngumu. Ndio maana mtoto wao wa kiume amerudi nyumbani kutoka kwenye mji mkuu wa nchi ya kigeni, kwa ajili ya kuchukua majukumu hayo. Alipokuwa Ulaya alisomea mambo mengine tofauti kabisa – alisomea famasia.

## **13. O-Ton Edmund Mbroso**

Hata sijuti. Sijutii chochote katika maisha yangu, kurudi kwangu naona nimechukua hatua inayofaa. Mimi ni raia wa nchi hii, kama nimejifunza kitu basi kwanza nafaa nirudi Ghana ili nitumie ujuzi huo kwa manufaa ya Waghana. Sidhani kama Uingereza inanihitaji zaidi kuliko Ghana. Kwa sababu huko Uingereza wapo wafamasia wengi ambao kiwango chao cha elimu kiko sawa na changu. Ghana haina watu wengi kama mimi. Pili: hii ni nchi yangu. Ninajivunia nchi yangu – Nilihitajika nirudi hapa. machache niliyojifunza huko Uingereza – niyalete hapa kusaidia

maendeleo ya watu wangu! Tunazungumzia kuhusu ushindani na nchi za Ulaya – kusema kweli ni muhimu kama raia, tutoe msaada wetu pia. Machache tunayoyajua, tuyalete nyumbani. Na hivyo ndivyo ninavyofanya mimi. Nafikiri ninafanya hivyo kwa ajili ya kuisaidia nchi yangu.

#### **14. Narrator:**

Jibu lake sio rahisi kulifahamu. Kwa nini anataka kuisaidia nchi yake, wakati ambapo ameshasema kuwa hali si nzuri? Labda anapuuza hali halisi ilivyo, anafafikiri kwamba huenda mambo yakatengemaa?

#### **15. O-Ton Edmund Mbroso**

Ndio na hapana. Ndio kwa sababu hapa Ghana, nina familia kubwa. Na wakati wote mimi hufikiri kwamba ninapokuwa na familia yangu karibu, ninaburudika na kupumzika. Ninajisikia vizuri zaidi kufanya kazi hapa Ghana. Hali ni ngumu kidogo kufanya kazi kule Uingereza. Unafanya kazi kulipia bili zako tu! lakini Ghana, unapata muda wa kupumua kidogo. Sio eti ninashauri hivyo, la. Kwa kawaida hivyo ndivyo ilivyo. Yaani hupati shinikizo la kukufanya ujipinde kwa kazi – licha ya kwamba ninafanya bidii katika kazi yangu. Ninafanya kila ninaloliweza – lakini sitaki kusukumwa pia. Ninaamka asubuhi, na ninafanya bidii kutimiza mengi katika saa 24, kwa hivyo sitaki kusukumwa zaidi.

#### **Scene 2:**

**16. SFX Guled at the hotel, is on the phone, speaking Somali and English**

**17. Narrator:**

Tuko hotelini, Mogadishu, mji mkuu wa Somalia huko Afrika mashariki. Kijana ambaye wakati wote anatumia simu yake ya mkononi, anazungumza Kiingereza na Kisomali. Kiingereza chake utadhani ni mzaliwa wa Uingereza. Guled Abdisalem ana miaka 32 na ameishi takriban nusu ya umri wake katika mji wa London. Amerejea Mogadishu, tangu wiki nne zilizopita.

### 18. **O-Ton Guled Abdisalam**

Bila shaka kuna hatari hapa. Hatari sana, na iwapo tutatathmini hali ya hatari – basi nitasema ni mia na zaidi”, (laughing), kwa hivyo eneo hili ni sawa na kusema ni eneo ambalo halifai mtu kufika. Lakini tena: Hapa kuna watu. Na hii ni nchi. Huwezi kufanya mambo kiurahisi halafu ukafikiri kuwa mambo yatakuwa sawa – hatari iko kila mahali.

### 19. **Narrator:**

Guled huenda akawa amerudi na mtazamo wa kijuu juu kutoka Uingereza, mtazamo ambao wazungu wanafahamika sana kuwa nao. Haoni kama mambo hayakukaa sawa kama yanavyoonekana. Ingawa mjini Mogadishu hatari ipo kiwango cha juu kuliko sehemu nyingine yoyote duniani. Kwa karibu miaka 20 sasa, tangu mwaka 1991, Somalia haijawa na serikali ambayo imefaulu kudumisha utulivu katika nchi hiyo. Ghasia na vitendo vya uvunjaji sheria vimezagaa. Ijapokuwa serikali mpya ilichukua mamlaka, muda mfupi tu kabla kurudi kwake Guled, serikali hiyo haijafaulu hata kuudhibiti mji mkuu, sembuse kuleta utulivu katika nchi nzima. Lakini Guled ana imani kubwa na serikali hiyo mpya. Na ndio maana amerudi kutoka Uingereza.

### 20. **O-Ton Guled Abdisalam**

Sijawahi kufikiria kuwa bilionea, sijafikiria kupata fedha nyingi, kila mara mimi nafikiria juu ya kumsaidia mtu mwingine. Kutumia elimu niliyo nayo kwa kutoa mchango wenye manufaa duniani. Nadhani ninaifanya kazi hiyo, ni ndoto niliyoiota kila siku: Kurudi hapa na kuanzisha vitu ambavyo nafikiria nina uwezo wa kuvifanya. Kuwahamasisha watu na kuzungumza na vijana, kuwaeleza tofauti baina ya vita na amani. Tofauti baina ya kuishi kwa amani na kuishi kwenye mapigano.

### **21. Narrator:**

Sababu iliyomrudisha mjini Mogadishu hapo mwezi February 2009, ni mwito alioupokea kutoka kwenye ofisi ya waziri mkuu. Guled alipigiwa simu akiwa mjini London na kufahamishwa kuwa amepewa nafasi ya kuwa msemaji na mshauri wa mambo ya habari wa waziri mkuu. Guled Abdisalam ni mwandishi wa habari wa kujitegemea na amekuwa ni mtu maarufu nchini Somalia. Amewahi kutengeneza filamu kuhusu vita vya nchini mwake kwa niaba ya shirika la utangazaji la BBC. Alirejea nchini Somalia mara kwa mara kwa ajili ya kufanya utafiti na kujifahamisha zaidi iwapo angeamua kurudi nyumbani kabisa. Alifunga mizigo yake baada ya kupata simu ile.

### **22. O-Ton Guled Abdisalam**

Sababu iliyonifanya kurudi wakati huu, na pia kuamua kuwa nitakaa hapa, ni kwa sababu ninaona kuna mafanikio. Mafanikio ninayo yaona ni kwamba watu sasa wamebadilika, sio watu nilio waona hapo mwanzo. Wakati wote nilitafuta kuona mafanikio kama haya.

### **23. Narrator:**

Baadhi ya wawakilishi wa serikali mpya pia wamerejea kutoka nchi za nje. Mkuu mpya wa Guled, waziri mkuu Omar Abdirashid Ali Sharmake,

ana passpoti mbili ya Canada na ya Somalia, alikuwa zamani ni balozi katika umoja wa mataifa, alihudumu kwa miaka tisa katika nchi tafauti za Kiafrika ambazo zilikumbwa na migogoro. Guled mwenyewe, alikwenda mjini London kwa mara ya kwanza alipokuwa na miaka 14. Wazazi wake walimpeleka kwenda kuishi na ndugu, huku wao wakiishi Misri. Familia hiyo ililazimika kuishi uhamishoni kwa ajili ya vita vya nchini Somalia. Ingawa anasema kuwa wazazi wake hawakuteseka. Lakini hawakupata fursa ya kupata elimu:



**24. O-Ton Guled Abdisalam**

Walikuwa na mawazo ya kutaka watoto wao wawe na maisha bora; wajukuu zao na vizazi vijavyo walitaka viwe na mtazamo na mawazo tafauti. Kwa hivyo walikuwa na kiu ya elimu. Walinipangia maisha yangu, haukuwa mpango wangu, mimi kuwa Mwingereza, kuwa raia wa Ulaya, lakini yote hayo yaliwezekana.

**25. Narrator:**

Guled Abisalam ana shahada mbili. Yeye ni mwandishi wa habari, na pia ana shahada ya uzamili yaani “ Master's” kwenye masomo kuhusu Afrika ambayo aliipata mwaka 2007. Wakati wote aliokuwa Uingereza hakuisahau Somalia.

**26. O-Ton Guled Abdisalam**

Wazazi wangu na ndugu zangu, kila mara walikuwa wakisema: Ukienda Somalia, utafanikiwa zaidi, utaona mwanga mbele yako ukienda huko, – watu wako wanakuhitaji. Na kutoka wakati huo, Somalia hapakuwa mahala mtu alipotaka kuishi. Ukiangalia habari, ukiangalia wakimbizi na mambo yote hayo, ilikuwa vigumu. Nao wazazi wangu pia walikuwa ni wazalendo. Baba yangu na mjomba wangu waliniambia: Unajua? Tunataka Somalia iwe na maisha bora. Na walikuwa wakinieleza jinsi Somalia ilivyokuwa zamani. Kwa hivyo walisema: Unajua, nchi hii inahitaji watu werevu ambao wanaweza kurudisha hadhi ya nchi hii. Ndio maana kila mara ninasema: Ndio, Nina mahala ambapo ninaweza kuwa muasisi. Mtu anayeweza kuanzisha kitu ambacho hakikuwepo hapo awali. Nina matarajio kama hayo. Na sio mimi tu. Lakini Wasomali wengi.

---

## **Outro:**

Ni hayo tu kwa leo katika makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu Uhamiaji. Mwandishi wetu alikuwa ni Bettina Rühl. Asante kwa kutusikiliza. Iwapo ungependa kujifahamisha zaidi kuhusu kipindi hiki au ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki ama vipindi vingine vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, tafadhali tembelea kwenye mtandao wetu.

Anuani yetu ni: [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe)

Usikose kujiunga nasi wakati ujao kwenye makala nyingine. Kwaheri.